# MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA MTIHANI WA KISWAHILI 102/2. KCSE 2024

**1. UFAHAMU**

**(a) Mitazamo ya watu wa mijini kuhusu watu wa kijijini**

(i) Wanawaona watu wa kijijini kama wasiojua kutekeleza mambo/ Ni wajinga.
(ii) Wanawaona kama wasiojiendeleza/ Wako nyuma/hawana maendeleo.
(iii) Huwaona kuwa wachafu ( Kupangusa mkono kwa nguo baada ya salamu).

**Hoja 2x1=2**

**(b) Jinsi tabia za watu wa mjini zilivyoathiri watu wa kijijini**

(i) Waliandaa kikao kuzungumzia tabia za watu wa mjini.
(ii) Walikerwa na tabia za watu wa mjini kuwaona kama watu wasioweza kufanya baadhi ya mambo na kuwa hawana maendeleo/hawaendelei.
(iii) Hawakupendezwa na mavazi/viguo vifupi vya wasichana wa mjini- viguo hivyo vinaona mpaka ndani.
(iv) Hawapendi wanavyozungumza lugha ya kigeni na wenyeji/ Wenyeji hawakuelewa lugha hiyo/Wenyeji walitatizika katika mawasiliano.
(v) Watu wa mjini walikataa kula vyakula vya kienyeji (mrenda na mchicha).
(vi) Watu wa mjini walijifanyia kazi badala ya kuwapa kazi hizo.
(vii) Tabia za watu wa mjini ziliwafanya wazozane/wavutane, kwa mfano Muna na Kwini.
(viii) Watu wa mjini walikitawala kijiji kama ni chao.
(ix) Waliogopa kuwasalamia watu wa mjini. Watu wa mjini waliwaona kuwa wachafu- walipangusa mkono baada ya kusalamiana. **Hoja 5x1=5**

**(c) Manufaa ya likizo zinazodhihirika katika kifungu**

(i) Huwawezesha kufanya kazi zingine/tofauti. *Bila zingine au tofauti=0 mk.
(ii) Huimarisha misuli.
(iii) Huchangamsha ubongo.
(iv) Huwezesha mtu kuwa katikma hali nzuri ya kuanza tena kazi anaporejea afisini.
(v) Hufanya viungo vya mwili kuwa vyepesi.
(vi) Hukumbusha mtu asili yake.
(vii) Huwakumbusha watu (kuwatanabahisha) kuhusu umuhimu wa kufanya kazi za nyumbani. **Hoja 4x1=4**

**(d) Sifa mbili za msimulizi wa kisa hiki**

(i) Ni mbaraza/mpenda watu/mwenye upendo (Alipenda kujumuika na wenzake).
(ii) Mtetezi- anamtetea Bwana Tambo.
(iii) Mwenye kumbukumbu nzuri- anakumbuka aliyoamiwa na Bw. Tambo.
(iv) Ni mchanganuzi/mwelewa wa mambo/Mmakinifu.
(v) Mwenye msimamo dhabiti. **Hoja 2x1=2**

**(e) Maana ya maneno kulingana na kifungu**

(i) **alijikatia kauli**- alijiamuliaalijifanyia uamuzi. *Bila viambishi –aliji- 1 mk+kosa la s.

(ii) **yamenoga**- yamepamba moto/yamekolea/yamezidi/yamekuwepo kwa muda/yameshamiri/yameselelea/yameshika/yamechacha. *Bila viambishi –yame- 1 mk+kosa la s. **Hoja 2x1=2**

**2. UFUPISHO**

(a) **Fupisha aya nne za mwanzo kwa maneno 100**.

1. Muziki una nafasi kubwa na muhimu(isiyolinganishika) katika maisha ya watu.
2. Muziki ni njia mbadala ya binadamu kujieleza.
3. Binadamu hufaidi uhondo unaoletwa na muziki.
4. Burudani ya muziki si ghali/Burudani ya muziki ni rahisi.
5. Ni rahisi kuhifadhi na kusambaza muziki kwa sababu ya teknolojia.
6. Muziki huwaburudisha watu katika shughuli na sehemu mbalimbali.
7. Watu wa mjini hupenda burudani ya muziki kwenye maeneo ya muziki mtamu.
8. Hapa utaona wanamuziki wakiwa wamezaama katika usanii wao.
9. Kwa kucheza muziki ,watu huondoa huzuni/Muziki humvua mtu huzuni.
10. Wanamuziki hufurahi kwa namna ambavyo watu wanavyopokea sanaa yao.
11. Wasanii hutumia muziki kama kitegauchumi/Muziki huwapa ajira/Huwaletea kipato.
12. Muziki ni nyenzo (njia) kuu ya kutoleaa mawaidha/Huipa jamii mwelekeo.
13. Nyimbo za ibada huitangaza dini.
14. Muziki huhifadhi utamaduni wa watu/Huendeleza utamaduni/Ni balozi wa utamaduni. **Hoja 9x1=9**

**(b) Fupisha aya mbili za mwisho kwa maneno 70.**

1. Muziki unaonyesha dalili ya kudorora/kudumaa.
2. Wanamuziki wa awali walikuwa mahiri wa kupiga vyombo vya muziki.
3. Wasanii wa sasa hawapigi vyombo bali hutegemea midundo iliyorekodiwa.
4. Siku zijazo hapatakuwa na wajuzi wa zana za muziki/Hatutaweza kuwapokeza chipukizi maarifa ya watangulizi.
5. Wasanii wa kisasa hutoa nyimbo haraka.
6. Nyimbo hizo hukosa umakinifu wa ujumbe na usanii.
7. Kuna nyimbo za kisasa zinakosa heshima.
8. Hadhira huona aibu kusikilioza nyimbo zisizo za heshima.
9. Hadhira hususia nyimbo zisizo za heshima..
10. Nyimbo zinazozalishwa haraka hufa mapema. **Hoja 5x1=5**

**M**-a- 9

-b-5

Utiririko 1=15-shz

3. MATUMIZI YA LUGHA

(a) Neno, taa, saa, ufizi, lala, rafu, dawati, ndoa, anza, jinsi, nk.
/n/ /t/ /s/ /z/ /l/ /r/ /r/ /nd/ /nz/ /ns/. **1x1=1**

Tanbihi: Kuali sauti zote mwambatano za ufizi.

(b) U-li-o-**<u>pa</u>**-ndwa /ulio**'**pandwa [Shadda huwekwa kwa silabi ya pili kutoka mkono wa kulia kurudi mkono wa kushoto]. **1x1=1**

(c) –vi- ngeli/idadi/wingi/kiima
ki- masharti/hali/wakati/njeo
m- nafsi/mtendwa/yambwa/shamirisho/kipozi/umoja/idadi/yeye/yambwa tendwa/shamirisho kipozi.
i-kauli/mnyambuliko/kiendelezi/jinsi
a-kiishio/kimalizio/kauli tenda/kitamatishi **Vitahiniwa 4x1=4**

*Mzizi si kiambishi[basi mzizi uachwe nje]

*Mizizi ni miwili- Vut- i-a- [m- kitondo/mtendewa/yambwa tendewa]
-Vuti-a

(d) Kuandika sentensi upya

(i)
- Mabaharia walifika bandarani <u>baada ya</u> kusafiri kwa wiki moja.
- Mabaharia walifika bandarini <u>baada ya</u> safari ya wiki moja.
- <u>Baada ya</u> kusafiri kwa wiki moja mabaharia walifika bandarini.
- <u>Baada ya</u> safari ya wiki moja mabaharia walifika bandarini.
- Mabaharia walikuwa wamesafiri kwa wiki moja <u>kabla ya</u> kufika bandarini.
- Mabaharia walisafiri kwa wiki moja <u>hadi</u>/<u>mpaka</u> wakafika bandarini.

*Vihusishi vingine- hata/kisha/halafu. **1/0**

(ii)
- Uvumbuzi wa huduma huduma hiyo ulimfanya afisa husika apandishwe cheo na mkurugenzi.
- Kuvumbuliwa kwa huduma hiyo na afisa husika kulifanya mkurugenzi ampandishe cheo.
- Mvumbuzi/mvumbuaji wa huduma hiyo ambaye ni afisa husika alipandishwa cheo na mkurugenzi.

*Majibumengine yatumie: Uvumbuaji. **1/0**

(iii)
- Wanakijiji wa**<u>ki</u>**weka mikakati ifaayo, watajitosheleza kwa chakula.
- Wanakijiji wataka**<u>po</u>**weka mikakati ifaayo, watajitosheleza kwa chakula.
- **<u>Ikiwa/endapo/Iwapo/Kama</u>** wanakijiji wataweka mikakati ifaayo, watajitosheleza kwa chakula.
- Wanakijiji **<u>ambao</u>** wataweka mikakati ifaayo, watajitosheleza kwa chakula.
- Wanakijiji wataka**<u>o</u>**weka mikakati ifaayo, watajitosheleza kwa chakula.
- Wanakijiji wataweka mikakati ifaayo **<u>na</u>** kujitosheleza kwa chakula. **1/0**

(iv)
- Shazi siko barabara hiyo itapitia/itakakopitia.
- Shazi haitapitiwa na barabara hiyo.
- Shazi siko ambako barabara hiyo itapitia.
- Shazi haitapitiwa na barabara hiyo.

*Matumizi yote ya **po/ko/mo** yakubaliwe.

(e) Vihisishi vya kuibua hisia :

(i) Kinyume na matarajio- Kumbe!/alaa!
Kumbe! Mzee huyu ni tajiri hivi! **1//0**

(ii) Kutaka kitu kinusurike- Hamadi!
Hamadi! Kikombe hicho kitavunjika.
Hamadi! Gari hilo litagonga pikipiki. **1/0**

(f) **Kasha** hilo lililotengenezewa kiwandani/viwandani na **fundi** huyo lilimnufaisha.**2x1=2**
*****Kiwandani /viwandani ikubalike. Kiwandani=ndani, viwandani=eneo la viwanda.
*****Mhimili ni **kasha** na fundi. Mf akikosea kwingineko apawe adhabu ya **s** au **h**.

(g) Maguo yenyewe yalihifadhiwa kwenye makapu.

- Majiguo yenyewe yalihifadhiwa kwenye majikapu. **2x ½ =1**

(h) Wachezaji **wangali/bado** wanafanya mazoezi. **1/0**

(i) <u>Soko la kijiji chao</u> lilisafishwa na vijana. **2/0**
*Kilisafishwa- Mf aondolewe kosa la sarufi.

(j) -"Mnahitaji kuwapeleka watoto kwa chanjo dhidi ya polio Ijumaa itakayofuata/ijayo/ambayo itafuata", Chifu/chifu aliwakumbusha walezi.
-Chifu aliwakumbusha walezi, "Mnahitaji kuwapeleka watoto kwa chanjo dhidi ya polio Ijumaa ijayo/ambayo itafuata/Ijayo."
-Chifu: (akiwakumbusha walezi) Mnahitaji kuwapeleka watoto kwa chanjo dhidi ya polio Ijumaa ijayo/itakayofuata/ambayo itafuata. **2/0**
*Mf akiweka neno walezi kwa usemi ni 0 mk.

(k) Maana tatu ya sentensi: Mandila aliwatangazia chao.
**Tanbihi**: Utata unatokana na:

1. Kauli- 1. Kwa niaba ya/badala ya

   2. kwa manufaa/faida ya/kwa ajili ya/kwa sababu ya

   3. Aliwatumia kutanganza (nyenzo). Km, Wanaovaa fulana za Safaricom hutangaza vitu za Safaricom.

2. Chao (kivumishi kimilikishi) 1. Kutangaza kitu cha Mandila na wengine

   2. Kutangaza cha wengine bila Mandila

   3. Kutangaza cha watu wasiojulikana (ambao hawapo)

3. Shamirisho- "wa" /nafsi ya 1. wao 2. ninyi/yinyi
4. Chao- kifaa. **3x1=3**

(l) Matumizi ya mawili ya <u>kistari kifupi</u> kando na kutenga silabi na kudokeza hoja.

- Kutenga maneno ya ufafanuzi katika sentensi.
  Maafisa wote-wale walioajiriwa mwaka huu- watapelekwa kwa mafunzo.

Mbwa wao-aliyenunuliwa juzi- amepotea

- Kutenga tarehe- Tutaondoka tarehe 10-2-2025.
- Kutenga kipindi- Rais Moi alitawala 1978-2002.
- Kudumisha sauti/silabi- alikimbia-a-a-a
- Kuunganisha maneno mawili/nomino mwambatano- Mweka- hazina (Mweka hazina), Bata-mzinga (bata mzinga), askari-jela (askari jela)
- Mwishoni mwa sentensi kuonyesha kuwa kuna silabi iliyoachwa.

Km. Alimpa-
tia chakula.

- Kuonyesha ngeli. Km, Mwalimu alitufundisha ngeli ya A-WA leo asubuhi.
- Kuonyesha kuwa kuna kipashio kilichoachwa katika neno.
  Km, Watu –tatu wamefika shuleni.
- Kuonyesha mfumo wa elimu. Km , Mfumo wa elimu nchini Kenya ni 8-4-4.

**2x1=2**

(m) Tunga sentensi yenye muundo huu: KN(N+V)+KT(T+KH)+U+KN(0)+KT(T+E)

- Mlezi wake alimpenda kwa dhati lakini hakumthamini kamwe.
- Mlezi wake alimwelekeza ndani ya nyumba lakini alitoka nje.
- Mtoto mtundu alipigwa na mwalimu na kunyaza jii. **2/0**

*****Sentensi lazima iwe ambatano. **Tanbihi**: Hakiki majibu ya wanafunzi ipasavyo.

(n) Kwa jamii- mahali/pahali/eneo/kihusishi/kuhusisha
Wenyeji kwa wageni- pamoja na/kujumuisha/kuunganisha/kiunganishi. **2x1=2**

(o) mafuta- YA-YA/YA/A-WA/-WA
kwato- U-ZI/I-ZI/ZI **2x1=2**

(p) Tuta aliwaangukia miguuni wazazi wake.
-Tuta aliwaomba radhi /aliwataka radhi wazazi wake.
Tuta aliwashika miguu wazazi wake. **1/0**
***Tanbihi**: sentensi si lazima.

(q) Kusimulia ni kwa kutamba:
Na heshima/staha/nidhamu ni kwa adabu na thabiti/madhubuti/jadidi/tisti/ngangari/kabambe/hadidi/mithaki/kidete ni kwa imara. [*mf atoe visawe vya maneno aliyopewa]. **2x1=2**

(r) Methali ambayo huambiwa mtu ambaye anadharau vitu duni ambavyo vinaweza kumfaa wakati wa shida.

- Usiache mbachao kwa msala upitao.
- Gae huwa chombo wakatiwe.
- Matikiti na matango ni maponya njaa.
- Mchama ago hanyeli, huenda akauya hapo.
- Usitukane mkunga na uzazi ungalipo.
- Kiserema kimelima kimeshinda jembe zima.
- Kiserema hulima kikashinda jembe zima.

- Usisahau ubaharia kwa sababu ya unahodha.
- Usinyie kambi huenda ukauya hapo.
- Usidharau madafu maembe ni ya msimu.
- Akipa si mbi japo ya kumbi siku ya kivumbi hutia motoni.
- Ukipata chungu kipya, usitupe cha zamani.
- Tambara mbovu hutunzwa vyema.
- Ganda la mua la jana chungu kaona kivuno. **1/0**

(s) Vitate- **kazi** na **kasi**.

- **kazi**- shughuli anayofanya mtu.
  - mapambo
  - mshono wa shingoni katika kanzu ya darizi.

  **kasi**- upesi sana/haraka mno/mbio sana
  - tendo la kusokota uzi ili kupatikane mshipi au nyuzi za nyavu. **2x1=2**

  *Mf asilazimishe tu sentensi. Akitumia neno kazini=0 mk.

  **Tanbihi**: Mf lazima atunge sentensi na iwe moja. Bila sentensi=0 mk.

(t) Malipo anayolipa mtu ili kuachiliwa kwa muda kesi ikisikizwa:

- Dhamana/aburani/fungo/kafala.

  *Mf akiandika thamana= 1 mk na adhabu ya kosa la **h**.

**4. ISIMUJAMII**

(a) Bainisha sajili- Sajili ya biashara/Sajili ya matangazo/Tangazo la biashara/Kutangaza biashara/Tangazo la kutangazia biashara. **1x2=2**

*Ithibati si lazima.

(b) Sifa <u>nane</u> za sajili hii kwa kurejelea makala.

1. Matumizi ya lugjha shawishi/ya kusihi. Km, rafiki yako…/Usijikune kichwa, nk.
2. Matumizi ya balagha/mubalagha. Km, …mahitaji yamekujaa pomoni?
3. Mazungumzo yakuhusisha hadhira moja kwa moja. Km, …mahitaji yamekujaa pomoni?, Usijikune kichwa.
4. Lugha ya maelekezo/maelezo .Km, unachohitaji ni kubonyeza vitufe vya rununu yako.
5. Lugha ya kumwaminisha mteja kuwa ana mahitaji. Km, Mahitaji yamekujaa pomoni?
6. Lugha inayojenga ukuruba/utangamano kati ya mtangazaji na mteja. Km, Mpenzi mteja/ Rafiki yako.
7. Lugha ya heshima/adabu/upole/unyenyekevu. Km, Rafiki yako.
8. Matumizi ya uradidi/urudiaji/takriri/kurudia/usambamba. Km, Mpango unaojali watoto wako/mpango unaojali mfuko wako./..bure.
9. Matumizi ya chuku/kutia chumvi. Km, Mpango wa kusuluhisha matatizo yako yote.
10. Kuchanganya ndimi/lugha/misimbo. Km, Pata shopping bure!

11. Msamiati wa kibiashara/maalum/teule/msamiati wa kipekee. Km, mteja, mkopo,nk.
12. Nidaa. Km, Usijikune kichwa!
13. Nahau/misemo/semi. Km, Usijikune kichwa/ Meza mate/yamejaa pomoni,nk.
14. Tashbihi/Tashbiha/mshabaha. Km, Ni kama kumeza mate.
15. Tashihisi/Uhaishaji/Uhuishi. Km, Mpango unaojali, Rafiki yako Shirika la Jiimarishe.
16. Kuhamisha ndimi/msimbo/lugha. Km, Ni kama unapewa bure! Absolutely free!
17. Taswira. Km, kuponyeza vitufe. **Hoja 8 za kwanza x1=8**

    *kutaja ½ , mfano ½ . Tanbihi: Akikosa (a) na (b) pia anakosa (0 mk)